Toleo la sita

Julai—Septemba 2007

Banana Investments Limited

Mbiu ya Banana

YALIYOMO

BOHARI YA KUDUMU KUJENGWA KIBAMBA DAR ES SALAAM	2
MAONYESHO YA NANENANE 2007	2
AJIRA MPYA KAMPUNI YA BANANA	3
MKUTANO MKUU BANANA SACCOS 2007 WAASHIRIA MAFANIKIO	4
MAADHIMISHO YA SABASABA 2007	4

BODI YA WAHARIRI

Augustine S. Mnja—Mwenyekiti

Michael D. Bessa– Katibu

Adolf R. Olomi—Mjumbe

Alphonsina A. Olomi– Mjumbe

Ibrahim Shigela– Mjumbe

Adolf M. Mlay– Mjumbe

MAWASILIANO :*Banana Investments Limited*

Makao Makuu Oloirien Village, SLP 10123 ARUSHA, Simu 0272506475, 0754224440, 0754888470. Fax 0272501549. Email banana@bol.co.tz

Dar es Salaam Depot: Manzese, kati ya Moshi Hotel na Lambo Bar, SLP 79407 Dar es Salaam, Simu 0222774276, 0746707983, 0784774148.

Rombo Depot: Tarakea, SLP 105 Tarakea, Simu 0787074436.

Tanga Depot: Barabaraya 4, karibu na Msikiti wa Vohora, SLP 5150 Tanga, Simu 0272646134.

Pichaya Mkunguwa Ndizi iliyopamba Banda la Banana Investments Limited -Nanenane 2007

Mbiu ya Banana

Jarida lisilolewako na Banana Investments Limited, Toleo Na.6, Julai—Septemba 2007

BOHARA YA KUDUMU KUJENGWA KIBAMBA DAR ES SALAAM

Hivi karibuni kampuni ilinunua kiwanja eneo la Kibamba, jijini Dar es Salaam. Maandalizi ya kujenga bohari ndani ya kiwanja hicho yako mbioni na, endapo mambo yote yataenda ilivyopangwa, bohari hiyo ya kudumu itaanza kutumika mapema mwakani.

Kutokana na kiwanja hicho kuwa na eneo la kutosha, bohari mpya itakuwa na eneo la kutosha la kuegesha magari bila ya kubugudhiwa na msongamano wa magari. Vilevile kampuni inaweza kutumia eneo hilo kwa shughuli nyingine kwa faida yake. Kutokana na kupanuka kwa soko la bidhaa zake, kampuni inakaribisha wasambazaji wa bidhaa zake katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Morogoro. Wote wanaotaka kufanya biashara na kampuni yetu wanakaribishwa kutembelea bohari yetu ya muda iliyoko Manzese ambapo watapata maelezo na vipeperushi vinavyoelezea shughuli zetu. Pia wanaweza kuwasiliana kwa anwanini na simu zilizo ukurasa wa mbele wa jarida hili.

Imeandikwa na
Alphoncina A. Olomi

MAONYESHO YA NANENANE 2007.

Kampuni yetu ya Banana Investments ilishiriki katika maonyesho ya nanenane 2007 ambayo Kitaifa yalifanyika mkoani Arusha katika Viwanja vya Themi chini ya TASO, kanda ya Kaskazini.

Maonyesho hayo yalifunguliwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dr. Shein August 1, 2007 na kufungwa na Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania Mh. Kikwete siku ya kilele cha maonyesho hayo, August 8, 2007.

Maonyesho hayo yalishirikisha makampuni I mbalimbali ya ndani na nje ya Tanzania. Mwaka huu, tofauti na miaka mingine, banda letu ambalo ni jipya, kubwa na la kisasa lilipambwa kwa ustadi wa juu

Miongoni mwa wageni waliotembelea banda letu ni Waziri wa Kilimo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Dr.Makame ambaye alivutiwa na mkungu wa ndizi wenye urefu unaozidi kima cha mtu wa kawaida.

Ndani ya banda kulikuwa na komputa pamoja na runinga ambazo kwa pamoja zilionyesha shughuli mbalimbali za kiwanda kuanzia uhifadhi wa mazingira, uzalishaji na masoko.

Maonyesho haya yalikuwa na ushindani mkubwa sana kwani kila mshiriki alikuwa amejiandaa vizuri . Kampuni yetu ilifanikiwa kushinda nafasi ya kwanza katika usindikaji wa mazao ya kilimo na kuzawadiwa kombe .Vile vile pamoja na watu wengi kufika katika jingo letu tulipata bahati ya kutembelewa na viongozi mbalimbali kutoka sehemu mbalimbali mfano Waziri wa Uchumi na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Dr M. Makame na baadhi ya viongozi wa Serikali wa Chama na serikali na Wizara mbali mbali za serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Taasisi mbalimbali za Utangazaji kama Redio, TV na magazeti kwa ujumla wote walionja na kuvutiwa na bidhaa zetu.Hivyo kampuni ya Banana iliweza kujitangaza vizuri zaidi ndani na nje ya nchi yetu kupitia maonyesho hayo.

Imeaandikwa na
Denis W. Mkojera

Mbiu ya Banana

Jarida lisilowalo na Banana Investments Limited, Toleo Na.6, Julai—Septemba 2007

AJIRA MPYA KAMPUNI YA BANANA

Pamoja waajiriwa watano waliotajwa katika toleo lililopita, mwaka huu hadi Julai kampuni imeajiri katika idara mbalimbali kama ifuatavyo:

James E. Lyimo – Mhasibu Msaidizi

Bwana Lyimo ana Stashahada ya Uhasibu na uzoefu wa mwaka mmoja katika fani hiyo.

Venosa Sabas – Afisa Manunuzi

Bi Venosa Sabas ana Stashahada ya Ugavi (Materials Management) na uzoefu wa mwaka mmoja katika fani hiyo.

Jeyaprakash Kunjupillai – Meneja Uzalishaji Mwandamizi.

vana Kunjupillai ana Shahada ya .andisi na uzoefu kazini wa miaka 14 tika viwanda mbalimbali vya kuten-neza vinywaji.

Azza Mrinji. – Dereva Mauzo

Azza Mrinji ana Shahada Biashara na Usimamizi wa Masoko ya Chuo cha Nairobi, na Cheti cha mauzo – Dar-es-Salaam. Ana uzoefu wa miaka 12 (kumi na mbili) katika fani hiyo.

John Mgonja. – Dereva Mauzo

John Mgonja ana vyeti vya udereva kutoka VETA, utengenezaji wa magari na VTC. Anao uzoefu wa miaka sita (6) katika kuendesha magari makubwa na madogo.

Patrick S. Mushi – Afisa Utawala

Bwana Mushi ana Stashahada ya Rasilimali-watu na uzoefu wa mwaka mmoja katika fani hiyo.

Hashimu Adam. – Fundi wa kuosha Magari.

Hashimu Adam ana Leseni ya Udereva toka KIBO DRIVING SCHOOL – ARUSHA. Ana uzoefu wa kuendesha na kuosha magari kwa miaka miwili.

Martine K. Msofe. – Mlinzi

Martine Msofe ana Cheti cha Theology na Philosophy na ni mkufunzi wa Ulinzi. Ana uzoefu wa miaka 16 katika fani ya ulinzi.

Stephen J. Swai. – Dereva Mauzo.

Stephen Swai ana Leseni ya Udereva toka VETA (Vocation Education and Training Authority) – Moshi. na uzoefu wa miaka mitatu katika fani hiyo.

Witness Nkini. – Mlinzi.

Witness Nkini ana Cheti cha Ma-funzo ya Ulinzi toka katika kituo cha mafunzo cha Watch & Guard (T) Ltd Training School. Ana uzoefu wa mi-aka saba katika fani hiyo.

Abubakar Munishi. – Dereva Mauzo

Abubakar ana Cheti cha Udereva na uzoefu wa kuendesha magari ya aina zote (makubwa na madogo). Pia nao uzoefu wa miaka kumi ya uuzaji na usambazaji wa bidhaa mbalimbali.

Mbiu ya Banana

Jarida litolewalo na Banana Investments Limited, Toleo Na.6, Julai—Septemba 2007

MKUTANO MKUU WA BANANA SACCOS LTD 2007 WAASHIRIA MAFANIKIO

Mnamo Julai 7, 2007 Chama cha Akiba na Mikopo cha Banana, Banana SACCOS Limited, kilifanya mkutano mkuu wa mwaka. Mkutano huo ulikuwa wa kihistoria, kwani uliweka kumbukumbu nzuri kwa kuadhimisha miaka kumi ya chama (1997-2007), kupitisha taarifa zilizokaguliwa za fedha za miaka miwili, 2005 na 2006 na kuweka mipango endelevu ya kuimarisha chama. Pia, kwa mkutano kufanyika katika Ukumbi wa Gossa Banana Bar, kulianzisha ukurasa mpya wa kuelekeza mikutano mikuu nje ya eneo la kazi, jambo ambalo ni la hamasa na ufanisi mkubwa kiutendaji.

Baada ya kusomewa na kupitisha taarifa ya Bodi kuhusu maendeleo ya chama, mkutano mkuu ulipitisha taarifa ya hesabu za fedha zilizokaguliwa za 2005 na 2006 ambazo ziliwasilishwa na mkaguzi mkuu wa COASCO Mkoa wa Arusha, Ndugu Marwa.

Mkutano mkuu ulipitisha pendekezo la Bodi la kila mwanachama kuwekeza hisa zisizopungua shilingi 5,000/= kwa mwezi na ikakubaliwa zoezi hilo lianze Julai, 2007. Kima cha chini cha akiba kuwekezwa chamani na kila mwanachama kinabakia kuwa shilingi 5,000/= kwa mwezi. Kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya chama, hasa baada ya kuajiriwa kwa katibu wakudumu, mkutano ulipitisha pendekezo la Bodi la kuwekeza fedha za ziada katika miradi yenye kuzalisha faida.

Kuanzia Julai 2007 msisitizo umewekwa, ili kuelekeza mapato yote yatokanayo na hisa kwenye miradi na, endapo kitawezeshwa kukopa kutoka benki, chama kitatenga fedha kwa ajili ya akiba ya lazima kwa mujibu wa sheria ya Ushirika ya mwaka 2003.

Mkutano mkuu ulipitisha pendekezo la Bodi la kuomba ukomo wa madeni wa shilingi millioni hamsini (50,000,000/=) kwa kipindi cha mwaka unaoishia Desemba 31, 2007 kwa ajili ya kuboresha mfuko wakukopeshana. Wanachama waliaswa kutumia vizuri fursa hiyo, kukopa kwa busara na kurejesha mikopo kwa wakati.

Mkutano mkuu ulipitisha toleo la pili la masharti ya chama 2007 kupitiwa na Afisa Ushirika ya Manispaa ya Arusha kabla ya kutumwa kwa Mrajis kuthibitishwa.

Mkutano ulifahamishwa kuwa, baada ya kuajiri katibu, chama kinatarajia kuwa na mpango endelevu wa kuweka na kuhifadhi kumbukumbu za chama kwa usalama kwa njia ya kompyuta (soft copy) na hivyo kuhakikisha kuwa taarifa za fedha zinatoka na kuwasilishwa kwa wakati.

Imeandikwa na
Augustine S. Minja

MAADHIMISHO YA SIKUKUU YA SABASABA 2007.

Mwaka huu tulishiriki maonyesho ya 31 ya kimataifa ya Saba Saba ambayo yalifanyika katika Viwanja vya Mwalimu J.K. Nyerere, Kilwa Road Dar es Salaam kuanzia June 28 hadi July 8/2007. Tulijumuika na wasindikaji wa vyakula kuonyesha bidhaa zetu ndani ya Banda la SIDO.

Jambo la kufurahisha katika maonyesho haya ni kuona jinsi washiriki wengi walivyojitokeza toka ndani na nje ya nchi yetu. Zaidi ya 95% ya wageni waliotembelea banda letu wanafahamu vizuri bidhaa zetu na wengi walifurahia ubora wake na unafuu katika bei.

Banda letu lilitembelewa na watu mashuhuri wakiwemo mabalozi kutoka Korea, Marekani na Uingereza. Miongoni mwa wafanya biashara mashuhuri waliotembelea banda letu alikuwemo Mwenyekiti wa Makampuni ya IPP, Bwana Regnald Mengi.

Wafanyabiashara mbalimbali walivutiwa na bidhaa zetu na baadhi yao wakajitokeza kuomba kuwa wakala wa kuuza bidhaa hizo. Miongoni mwao kulikuwa na wakala mmoja kutoka Ifakara, wawili kutoka Dar es Salaam na wengine kumi kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania.

Imeandaliwa na
Adolf N.Mlay